MTANDAO WA KUZUIA UKATILI WA KIJINSIAG

**Siku 16 za Unaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia 2017**

**Karatasi ya Kazi ya Kampeni**

# KILA MSICHANA ANA THAMANI!

JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

## KILA MSICHANA ANA THAMANI! JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

Mwaka huu kampeni itaendelea kuzingatia haki ya kupata elimu wasichana na kutoa wito wa kuhakikisha kwamba wasichana wanabaki shuleni. Itaainisha ubaguzi wa kimuundo dhidi ya wasichana katika mifumo mbalimbali: kuanzia nyumbani, mazingira ya shuleni, na sera za serikali ambazo zinaathiri wasichana kupata elimu na changamoto zinazozuia kukamilisha elimu ya juu.

Kusudi la karatasi ya kazi ni kukusaidia kutafakari na kuyaoanisha katika mazingira yenu 'maombi' ya kampeni ya jamii yako. Maswali yaliyo katika majedwali hapo chini yataongoza tafakari yako na majadiliano katika timu yako. Ikiwa una shida ya kutumia karatasi kazi hii tafadhali soma info@preventgbvfrica.org kwa msaada zaidi.

### Tafadhali kumbuka:

1. Soma chapisho la Mapitio ya Kampeni kwanza na chapisho hili la karatasi ya kazi ya Kampeni kwa makini.

Tafuta na kusanya taarifa juu ya hali halisi katika jamii yako ukihusianisha na maswali kwenye karatasi kazi hapo chini. Unaweza kukusanya takwimu husika kutoka shule, kwa viongozi wa serikali na machapisho yanayotolewa.

3. Andaa mkutano wa Kampeni ya Siku 16 na wafanyakazi wenzako na toa taarifa za awali ulizoandaa. Jadili, fafanua, imarisha taarifa na urekodi maelezo katika jedwali la 3.

4. Kama kikundi, jadili na tambua 'hatua zinazohitajika' maelezo katika jedwali hili yatakusaidia kuandaa maombi maalum na kupanga kampeni inayolenga matokeo k.m. ahadi zitakazo tolewa na hatua zitakazo chukuliwa.

5. Soma na jadili maombi ya utetezi ya kampeni kwa undani na chagua mojapo ya ombi ambalo (kama shirika) utajiandaa vizuri kulipigia kelele katika jamii yako.

6. Fanyeni makubaliano kuhusu malengo mnayotarajia kuyafikia wakati wa kipindi cha kampeni na nini kitaonyesha mafanikio.

7. Pamoja na wafanyakazi wenzako, andaeni mpango kazi wa kina katika kipindi cha kampeni. Hakikisha shughuli mnazopanga zinalingana na malengo mnayotaka kuyafikia. Tumia Mwongozo wa Shughuli za Kampeni kwa ajili ya kupata mawazo zaidi.

8. Sasa uko tayari kuanza kampeni yako – Nakutakia kila la kheri!

# MAOMBI YA KAMPENI

Kampeni ya Mtandao wa Kuzuia ukatili wa kijinsia, inaungana na kauli mbiu ya dunia, tutaendelea kuangalia suala la elimu ya wasichana na kuwaomba wanajamii, wazazi, shule na watunga sera kuhakisha upatikanaji na kukamilisha elimu kwa wasichana na wanawake kuwa katika hali ya uwazi. Tunaainishasha haki za wasichana kupata elimu iliyo salama kwa wote, mashirika yanaweza kuchagua mojawapo ya masuala yaliyoainishwa au kujumuisha na masuala yafuatayo ambayo yanachangia kuleta vikwazo katika elimu ya wasichana kwenye jamii yenu na kutoa mwito juu ya hatua zinzotakiwa kuchukuliwa.

1. Upatikanaji wa elimu: hakikisha wasichana wote wanaandikishwa shuleni na kubaki shuleni mpaka wakamilishe elimu ya juu.
    a. Je, wasichana na wanawake wenye umri mdogo wanapata fursa sawa ya kupata elimu katika jamii yako?
        i. kuna uwiiano gani wa idadi ya wanafunzi wa kike na kiume katika ngazi mbalimbali za elimu katika jamii yako? Je! Mabadiliko ya uwiano hutokea katika ngazi za juu za elimu? Kwa nini? Ni vikwazo gani vinavyowapata wasichana katika kumaliza shule? Kwa mfano, wasichana / wanawake wenye umri mdogo katika jamii yako wanaolewa katika umri gani? Nini kinatokea wanapopata mimba? n.k.
        ii. Tunawezaje (kama wazazi, jamii na viongozi, walimu,watoa huduma wa afya, viongozi wa dini, viongozi wa serikali za mitaa, nk)? kuhakikisha kuwa wasichana wanabaki shuleni?
        iii. Je! Kuna sera zinazowabagua wasichana (yaani, kufukuzwa wasichana wanapopata mimba, nk) Je, sera hizo zinawezaje kubadilishwa? Mchakato utakuwaje? Nani anajukumu la kufanya hivyo?
    b. Hata wakati wasichana wanapokuwa wanapata elimu, je wanakuwa salama wanapokuwa shuleni?
    c. Je! Nimazingira gani yanawaweka wasichana hatarini mashuleni? (k.m.,unyanyasaji wa kijinsia, ngono kwaajili ya kufaulu mitihani, uonevu, ukosefu wa usafi wa mwili na mazingira, adhabu za viboko, nk)
2. Mfumo wa elimu. Unatoa changamoto juu ya mifumo ambayo inachangia ubaguzi na ukandamizaji unaosababisha kutokuwapo na usawa hali ambayo inawakabili wasichana. Hamasisha mitaala na vitabu vinavyohakikisha na kuonyesha usawa wa kijinsia na uhuru wa wasichana na wanawake.
    a. Je! Maudhui yanayofundishwa shuleni yanachangia ubaguzi wa wasichana na wanawake wenye umri mdogo? Je, shuleni hupanda mbegu za kutokuwepo na usawa wa mamlaka? Je, inahamasisha mawazo kwamba wavulana wana thamani zaidi kuliko wasichana? Je! haya yanaweza kubadilishwa?
    b. Je! Wasichana na wanawake wenye umri mdogo wanahamasishwa kushiriki katika shughuli zote kama wenzao wanaume? Ikiwa ndivyo, hii inaweza kusheherekewa? Ikiwa sio, hii inaweza kubadilishwa?
    c. Je! Kuna walimu na wasimamizi wa kike katika nafasi za uongozi mashuleni ndani ya jamii yako? Je, wana majukumu sawa? Je! Wafanyakazi wa shule ni mfano wa kuigwa katika suala la usawa wa kijinsia? jinsi gani Wanaweza kuboresha?

Kwa ujumla; Sisi wazazi, walimu, watendaji, wanajamii na viongozi, nk tunawezaje kufanya shule kuwa salama kwa wasichana? Je, ni mambo gani tunayoweza kufanya ambayo yange leta mabadiliko?

## Karatasi ya Kazi:

Tafadhali soma maswali hapo chini na utafute taarifa zinazokufaa uzikamilishe na kufanya kampeni yako ishughulikie mahitaji muhimu zaidi katika jamii yako.Tumia majibu yako ili kutengeneza maombi maalum ya jamii yako yanayolenga kupata mpango kazi na hatua zitakazoleta mabadiliko, kupitia shughuli mbalimbali unazopanga kuzifanya.

# KILA MSICHANA ANA THAMANI!

## JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

| 'Maombi' ya kampeni. | Maswali | Hali halisi ya jamii yako kulingana na swali. (*Tafadhali jaza kikamilifu sehemu hii*) | Hatua zinazohitajika – Je, ni hatua gani tunazoweza kuchukua ili kuleta mabadiliko? Nani atachukua hatua? (Tafadhali jaza sehemu hii) |
|---|---|---|---|
| **Hakikisha wasichana wote wanaandikishwa shuleni na kubaki shuleni mpaka wakamilishe elimu ya juu** | Je, wasichana na wanawake wenye umri mdogo wanapata fursa sawa ya kupata elimu katika jamii yako? | | |
| | kuna uwiiano gani wa idadi ya wanafunzi wa kike na kiume katika ngazi mbalimbali za elimu katika jamii yako? Je! Mabadiliko ya uwiano hutokea katika ngazi za juu za elimu? Kwa nini? | | |
| | Ni vikwazo gani vinavyowapata wasichana katika kumaliza shule? Kwa mfano, wasichana / wanawake wenye umri mdogo katika jamii yako wanaolewa katika umri gani? Nini kinatokea wanapopata mimba? n.k. | | |
| | Je! Kuna sera zinazowabagua wasichana (yaani, kufukuzwa wasichana wanapopata mimba nk)? | | |
| | Hata wakati wasichana wanapokuwa wanapata elimu, je wanakuwa salama wanapokuwa shuleni? | | |
| | Je! Nimazingira gani yanawaweka wasichana hatarini mashuleni? (k.m.,unyanyasaji wa kijinsia, ngono kwaajili ya kufaulu mitihani, uonevu, ukosefu wa usafi wa mwili na mazingira, adhabu za viboko, nk) | | |
| **Changamoto juu ya mifumo ambayo inachangia ubaguzi na ukandamizaji unaosababisha kutokuwapo na usawa hali ambayo inawakabili wasichana.** | Je! Maudhui yanayofundishwa shuleni yanachangia ubaguzi wa wasichana na wanawake wenye umri mdogo? Je, shuleni hupanda mbegu za kutokuwepo na usawa wa mamlaka? Je, inahamasisha mawazo kwamba wavulana wana thamani zaidi kuliko wasichana? Je! haya yanaweza kubadilishwa? | | |
| | Je! Wasichana na wanawake wenye umri mdogo wanahamasishwa kushiriki katika shughuli zote kama wenzao wanaume? Ikiwa ndivyo, hii inaweza kusheherekewa? Ikiwa sio, hii inaweza kubadilishwa? | | |
| | Je! Kuna walimu na wasimamizi wa kike katika nafasi za uongozi mashuleni ndani ya jamii yako? Je, wana majukumu sawa? Je! Wafanyakazi wa shule ni mfano wa kuigwa katika suala la usawa wa kijinsia? jinsi gani Wanaweza kuboresha? | | |